

## Uganda, Tanzania Wanahitaji Sera za Mabadiliko ya Tabia Nchi Zinazozingatia Jinsia NaWambi Michael



KAMPALA, Uganda, Nov 26 2015 (IPS) - Wanawake ni asilimia 80 ya nguvu kazi katika kilimo nchini Uganda lakini hata hivyo masuala ya jinsia hayaonekana sana katika sera za kilimo na mabadiliko ya tabia nchi.

Mabadiliko ya tabia nchi yanahitaji kuwa katika agenda ya juu ya nchi, kwa mujibu wa mradi unaoangalia sera za Uganda. unasema kuwa nchi hiyo haijaangalia kwa undani suala la mabadiliko ya tabia nchi katika mipango yake ya maendeleo ya kitaifa na kilimo, suala ambalo linapaswa kufanyiwa kazi kabla ya kuchelewa sana.

Mradi wa Sera za Mabadiliko ya Tabia Nchi (PACCA) unataka kutengeneza na kuunganisha sera na taasisi kuanzia ngazi ya kitaifa hadi serikali za mitaa kwa ajili ya kubuni na kutumia mifumo ya kuwa na chakula kinachostahimili mabadiliko ya tabia nchi nchini Uganda kwa kuwa sera zipo lakini zimetawanyika na hivyo kuhitaji kuunganishwa.

Edidah Ampaire, Mratibu wa Sera wa PACCA aliiambia IPS kuwa mbali na kukosa kuunganisha sera katika ngazi za kitaifa na kitaasisi, sera nyingi nchini Uganda zinahitaji kufanyiwa marekebisho ili kuingiza masuala ya mabadiliko ya tabia nchi na kilimo.

“Sera nyingi ziliandaliwa wakati ambapo mabadiliko ya tabia nchi hayakuwa suala kubwa. Kwa hiyo zinaonekana kuelekeza nguvu zaidi katika mazingira pamoja na kuwa katika undani wake zinazungumzia kuhusu usimamiaji endelevu wa rasilimali, jambo ambalo pia linasaidia wakulima kuwa na uwezo wa kukabiliana na mabadiliko lakini hawazungumzii kwa undani kuhusu mabadiliko hayo,” alisema Ampaire.

Mradi wa PACCA, unaoongozwa na Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo katika Nchi za Kitropiki (IITA), pia unafanya kazi nchini Tanzania. Alipoulizwa kuhusu hali nchini Tanzania, Ampaire alisema Tanzania haina tofauti na Uganda. “Hali nchini Tanzania inaweza kuwa mbaya zaidi ikilinganishwa na kile kinachofanyika nchini Uganda hasa katika ngazi ya serikali za mitaa na jamii,” alisema.

Ampaire alisema ushahidi nchini Uganda na Tanzania unaonyesha kuwa kwa wakati huu sera siyo tu kwamba zimegawanyika na kutekelezwa vibaya, lakini wahusika mbalimbali pia hawakuziratibu vizuri na majukumu yao hayapo wazi.

Nchini Uganda, sera kama ile ya Mabadiliko ya Tabia Nchi ya 2013, Sera ya Kilimo ya 2013 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa, Sera ya Jinsia Uganda 1997 zilifanyiwa tathmini.

Moja ya matokeo ya kushangaza kwa mujibu wa Ampaire ni kwamba sera zote hizo hazikuelezea masuala ya jinsia katika kukabiliana na madhara ya mabadiliko ya tabia nchi.

“Tunachokiona katika sera zenyewe ni kwamba hazihusiki na masuala ya jinsia kwa kiasi cha kutosha. Hazina vifungu vinavyozungumzia kuhusu makundi maalum. Na nadhani hili ndilo tatizo hasa katika ngazi ya kijamii,” Ampaire aliiambia IPS. “Zinapaswa kuweka mikakati ambayo inashughulikia kukosekana kwa usawa miongoni mwa makundi mbalimbali kama vile ya vijana na wanawake. Hii ni kutokana na kuwa nchini Uganda, asilimia themanini ya nguvu kazi ya kilimo inatokana na wanawake lakini hawapo mahali popote pale na hawana rasilimali,” aliiambia IPS.

Kwa upande wa Tanzania, Ampaire alisema Mawasiliano ya Awali ya Kitaifa (INC) na Mpango wa Utekelezaji wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi (NAPA) ulioandaliwa na Serikali ya Tanzania kwa ajili ya Mtandao wa Umoja wa Mataifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi (UNFCCC) haukingiza masuala ya jinsia.

Alisema ukiangalia suala la Uganda, mapendekezo yalitokana na utafiti ulioangalia mapengo katika sera za kitaifa na mikakati nchini Uganda. Utafiti unatoa mapendekezo ya kuboresha usawa wa kijinsia katika Kilimo Kinachozingatia Mabadiliko ya Tabia Nchi.

Ampaire aliiambia IPS kuwa Kilimo Kinachozingatia Mabadiliko ya Tabia Nchi lazima kizingatie jinsia na kisifaidishe kikundi kimoja tu cha watu.

Matokeo ya utafiti mwingine wa PACCA nchini Uganda juu ya jinsia na mabadiliko ya tabia nchi uligundua kuwa masuala ya mabadiliko ya tabia nchi yanachukuliwa kama mtambuka, na hivyo kutokupewa kipaumbele katika mgawo wa bajeti.

“Kuingiza masuala ya jinsia katika sera na mipango mingi iliyopitiwa kumeonekana katika vimbatanisho na wala siyo sehemu ya sera,” inasomeka sehemu ya ripoti yenye jina la “Jinsia na Mabadiliko ya Tabia Nchi Nchini Uganda: Madhara ya Sera na Mfumo wa Kitaasisi.”

“Jinsi masuala ya jinsia yanavyoangaliwa katika sera zinazohusiana na kilimo na mikakati nchini Uganda ni kama suala la jumla jumla. Kuna haja ya kuwa na uratibu wenye nguvu wa kisekta na uwajibikaji kutokana na kuwa shughuli za jinsia zinaangukia katika wizara na taasisi tofauti,” inasema ripoti iliyoandikwa na Edidah Ampaire, Wendy Okolo na Jennifer Twyman.

Katika wilaya za Masaka na Rakai kusini mwa Uganda zaidi ya asilimia tisini ya watu wanategemea kilimo kidogo kidogo. Kiasi kikubwa cha kilimo kinaendeshwa katika miteremko na mabwawa huku mashamba yakiwa na wastani wa ukubwa wa acre 2 na 3.

Kutokana na ongezeko la idadi ya watu kuna uvamizi wa mabwawa ya kando kando mwa mito ambayo yanalisha mfumo wa mto Nile, ikiwa ni pamoja na miteremko mikubwa na chemichemi za maji. Misimu miwili ya mvua katika eneo hilo imekuwa isiyotabirika na kuwa na mvua chache katika miaka ya karibuni.

Wakulima wanakabiliwa na matatizo ya upatikanaji wa maji na udongo usiofaa, na wanahitaji kutumia vizuri mvua lakini sera za kitaifa na za serikali za mitaa za kushughulika na mabadiliko ya tabia nchi hazizungumzii mahitaji maalum ya eneo hili.

Andrew Nadiope ni mtaalam wa mabadiliko ya tabia nchi kutoka Wizara ya Serikali za Mitaa nchini Uganda. Wizara yake imekuwa ikifanya kazi na PACCA kutathmini sera chini ya hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi katika ngazi ya chini. Tumegundua kuwa wakati wa kupanga tunapaswa kupanga tukiwa na mawazo ya mabadiliko ya tabia nchi kwani mara tu tunapoweka kumbukumbu za mahitaji maalum ya maeneo maalum, hatua za kukabiliana na hali zinaweza kulengwa kwa shabaha zaidi,” Nadiope aliiambia IPS.

Wilaya ya Rakai iliyopo kusini magharibi mwa Mkoa wa Kati nchini Uganda ina matatizo ya maji na maji ya chini ya ardhi katika eneo kubwa la wilaya hiyo yamejaa madini ya chuma. Wilaya hiyo yenye idadi ya watu inayokaribia nusu milioni inakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji. Serikali za mitaa kwa kushirikiana na serikali kuu imejenga zaidi ya maeneo ya kuchotea maji 1300 yenye visima vifupi na virefu lakini visima vingi havifanyi kazi kwa zaidi ya miaka mitano na vinaoenakana kutelekezwa kutokana na maji kuwa na chumvi.

Jude Sewankambo ambaye ni mkulima katika Kata ya Kagamba aliiambia IPS kuwa ujenzi wa visima hivyo unaonekana kuwa ni sehemu ya mipango mibovu. Alielezea kuwa wanajamii kama hawa hawakupewa taarifa wakati visima vikichimbwa. “Tuliishia kupoteza pesa katika miradi ya maji ya chini ya ardhi wakati tulipaswa kuchagua kuvuna maji ya mvua,” alisema.

Alisema mke na watoto wake mara kwa mara wamelazimika kutembea kilomita mbili kuchota maji ya mto.

Sewankambo aliiambia IPS kuwa yeye na mke wake waliambiwa kujenga matenki ya kuvuna maji ya mvua kunagharimu pesa nyingi. “Kama unataka tenki la ujazo wa mita kumi, unalipia karibu dola 800, na makinga maji ya uwezo wa lita elfu moja hadi elfu moja mia tano kwa dola 200. Watu wengi hawana uwezo kupata fedha hizi,” alisema.

(End)